JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI

# UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA YA UPOTOSHAJI ILIYOCHAPISHWA KWENYE MITANDAO YA KIJAMII

**DAR ES SALAAM: SEPTEMBA 25, 2025**

Kuna taarifa iliyochapishwa kupitia mitandao ya kijamii ya Instagram na Facebook kuwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili "imewafuta kazi wafanyakazi 200 kwakuwa haina fedha za kuwalipa" na kuchapisha barua ya mmoja wa wafanyakazi aliyepewa Notisi ya kusitishiwa ajira yake ya Mkataba.

Kutokana na taarifa hiyo, Uongozi wa Hospitali unapenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo;

a. Hadi kufikia leo tarehe 25 Septemba, 2025 Hospitali ina jumla ya wafanyakazi **4,326** ambapo kati yao **3,193** wapo Upanga na **1,133** wapo Mloganzila.

b. Aidha kati ya wafanyakazi **4,326** wenye ajira za masharti ya kudumu ni **4,075** na wenye mikataba ya muda mfupi ni **251** ambao wameajiriwa na Hospitali moja kwa moja au kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na wadau ndani ya Hospitali ambapo miradi hiyo inapofikia ukomo, ajira hizo husitishwa.

c. Tangu Januari hadi Septemba 25, 2025, Hospitali imepokea wafanyakazi wa ajira mpya **380** wenye masharti ya kudumu na kadiri Hospitali inavyopokea wafanyakazi hao, ndivyo inavyopunguza wafanyakazi wenye ajira za mikataba **(Volunteers)** kulingana na kada husika.

d. Katika kipindi hicho hicho, Hospitali ilitoa Notisi ya kusitisha mikataba kwa wafanyakazi 27 waliokuwa na ajira za mikataba ya muda mfupi **(Volunteers).**

e. Hivyo, taarifa iliyochapishwa na mitandao ya kijamii kuwa Hospitali imesitisha ajira za wafanyakazi 200 siyo za kweli.

f. Uongozi utaendelea kuajiri na kusitisha ajira pale itakapobidi kufanya hivyo kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za utumishi wa umma zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Imetolewa na;

*[signature]*

**Aminiel Aligaesha**
**MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO KWA UMMA**

Upanga Magharibi, Mtaa wa Kalenga, Kitalu Na. 10480/3, S.L.B 65000, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255-22-2151367-9, Simu: +255-22-2151351-2
Barua pepe: info@mnh.or.tz, Tovuti : www.mnh.or.tz